# WAKULIMA WA MARA CO-OPERATIVE UNION (WAMACU) LTD

**NAMBARI YA USAJILI. 5573**

## TIN Na. 138-950-433

## MASHARTI YA CHAMA

**OCTOBER, 2021**

SHERIA YA VYAMA VYA USHIRIKA
(SHERIA Na. 6 YA MWAKA 2013)

WAMACU LTD

**MASHARTI**

---

(*Yametungwa* c*hini ya kifungu cha 52 cha Sheria ya Vyama vya Ushirika, 2013)*

---

Masharti haya yameandaliwa na wanachama kwa kuzingatia marekebisho ya masharti ya vyama vya ushirika ili yaendane na matakwa ya Sheria ya Vyama vya Ushirika No.6 ya 2013.

**MASHARTI YA CHAMA KIKUU CHA WAKULIMA WA MKOA WA MARA (WAKULIMA WA MARA CO-OPERATIVE UNION "WAMACU" LTD).**

# MPANGILIO WA MASHARTI


| Sharti | Kichwa cha matakwa |
| --- | --- |

## SEHEMU YA KWANZA

## MASHARTI YA AWALI

| | |
| --- | --- |
| **1** | Kuanza kutumika kwa masharti |
| **2** | Tafsiri |

### SEHEMU YA PILI

### TAARIFA ZA CHAMA

| | |
| --- | --- |
| **3** | Jina la chama |
| **4** | Anuani ya chama |
| **5** | Mfungamano wa Pamoja |
| **6** | Eneo la shughuli za chama |
| **7** | Tarehe ya kusajiliwa na namba ya kuandikishwa |
| **8** | Mwaka wa fedha |

### SEHEMU YA TATU

### MADHUMUNI

| | |
| --- | --- |
| **9** | Madhumuni ya Chama |

## SEHEMU YA NNE

## UANACHAMA


**10** Sifa za uanachama

**11** Wanachama

**12** Taratibu za kujiunga na Chama

**13** Taarifa ya kukataliwa uanachama

**14** Kiingilio, Hisa, Akiba na Amana

**15** Kuteua Mrithi

**16** Kukoma uanachama

**17** Malipo na haki za mwanachama aliyejitoa au kufukuzwa uanachama

**18** Kusimamishwa na kufutiwa uanachama

**19** Kupokelewa tena kwenye chama

**20** Wajibu wa Mwanachama

**21** Haki za Mwanachama

**22** Matumizi ya stahili za mwanachama aliyekoma kuwa mwanachama

**23** Dhima ya mwanachama


## SEHEMU YA TANO

## FEDHA NA MALI ZA CHAMA

24 Vyanzo vya fedha

25 Mali za Chama

26 Mali za Chama kuwekwa Rehani

27 Ukaguzi wa Hesabu za Chama

**SEHEMU YA SITA**

**TARATIBU KUHUSU HISA, AKIBA, NA AMANA**

28 Uwekaji wa Hisa, Akiba na Amana

29 Utunzaji wa Kitabu cha Mwanachama

**SEHEMU YA SABA**

**UHIFADHI WA FEDHA ZA CHAMA**

30 Uhifadhi wa fedha za Chama

**SEHEMU YA NANE**

**MATENGO NA MGAO WA ZIADA**

31 Mfuko wa Matengo ya Kisheria

32 Mfuko wa Elimu na Mafunzo

33 Mgawo wa ziada halisi

**SEHEMU YA TISA**

**USIMAMIZI NA UONGOZI WA CHAMA**

**34** Mamlaka ya Mkutano Mkuu

**35** Mkutano Mkuu wa Mwaka

**36** Mkutano Mkuu wa Kawaida

**37** Mkutano Mkuu Maalum

**38** Notisi ya Mkutano Mkuu

**39** Akidi ya Mkutano Mkuu

**40** Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu

**41** Upigaji Kura katika Mkutano Mkuu

**42** Muhtasari wa Mkutano Mkuu

**SEHEMU YA KUMI**

**BODI YA UONGOZI, KAMATI YA USIMAMIZI NA AJIRA**

**43** Bodi ya Uongozi

**44** Kukoma Ujumbe wa Bodi

**45** Vikao vya Bodi ya Uongozi

**46** Muhtasari wa Vikao vya Bodi ya Uongozi

**47** Kazi za Bodi ya Uongozi

**48** Kazi za Mwenyekiti wa Bodi ya Uongozi

49 Kazi za Makamu Mwenyekiti

50 Sifa za Mjumbe wa Bodi ya Uongozi na wa Kamati ya Usimamizi

51 Meneja wa Chama

52 Kamati Mbalimbali za Usimamizi

53 Kazi za Kamati mbalimbali za Usimamizi


**SEHEMU YA KUMI NA MOJA**

**UANDAAJI WA SERA NA MIONGOZO YA CHAMA**


54 Ajira katika chama

55 Mkaguzi wa Ndani wa Chama

56 Chama kuandaa Sera na Miongozo


**SEHEMU YA KUMI NA MBILI**

**KUFUTWA NA UFILISI WA CHAMA**


57 Kufutwa kwa Chama

58 Ufilisi


**SEHEMU YA KUMI NA TATU**

**MASHARTI MENGINEYO**


59 Viongozi kutunza siri

60 Msemaji wa Chama

61 Mihuri ya Chama

**62** Chama kuungana na taasisi nyingine

**63** Bima ya Mali na Fedha za Chama

**64** Mabadiliko ya Masharti

**65** Utatuzi wa migogoro

**66** Mgongano wa Tafsiri ya Masharti

**67** Utakatishaji wa fedha

**68** Uwasilishaji wa Taarifa

**69** Ulinzi wa Mlaji

**70** Upashanaji wa Taarifa za Wakopaji

SHERIA YA VYAMA VYA USHIRIKA
(SHERIA Na. 6 YA MWAKA 2013)

# MASHARTI

(*Yametungwa* c*hini ya kifungu cha 52 cha Sheria ya Vyama vya Ushirika, 2013)*

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Kuanza kutumika kwa masharti

1 Masharti haya yatajulikana kama Masharti ya Chama na yataanza kutumika mara baada ya kupitishwa na kuidhinishwa na kusajiliwa na Mrajis

Tafsiri

2 Katika Masharti haya, isipokuwa kama muktadha unahitaji vinginevyo maneno yaliyoanishwa hapa chini yatakuwa na maana iliyotolewa:

a) **"Afisa"** maana yake ni mtu mwenye wadhifa wa kuchaguliwa au kuajiriwa katika Chama ambaye

atajumuisha Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wa Bodi, Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Usimamizi, Mjumbe Mwakilishi, Meneja Mkuu, Mhasibu Mkuu, Mkaguzi wa Ndani, Mhazini na Wajumbe wengine waliopewa mamlaka chini ya masharti ya chama;

b) **"Akidi"** maana yake ni idadi ya chini au toshelezi ya wajumbe wanaotakiwa kuhudhuria ili kikao au mkutano uwe halali;

c) **"Amana**" ni fedha ambayo mwanachama anaweka chamani na anaweza kuichukua wakati wowote anapoihitaji kwa mujibu wa sera;

d) **"Bodi ya Uongozi"** maana yake ni chombo kilichochaguliwa na wanachama kupitia Mkutano Mkuu kwa ajili ya kusimamia shughuli za kila siku za chama;

e) **"Chama"** maana yake ni Chama cha Wakulima wa Mara Cooperative Union (WAMACU) LTD kilichosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika;

f) **"Dhamana"** itakuwa na maana ya kinga kwa ajili ya mkopo ambayo inaweza kuwa nyumba, shamba, vyombo, Hisa za hiari, Amana, Akiba au mali nyingine itakayokubalika kutumika kwa kuzingatia sera ya

mikopo;

g) **"Hisa za uanachama"** ina maana ya sehemu ya umiliki wa mtaji wa chama ambayo inamilikiwa na mwanachama lakini haitakiwi kuzidi asilimia ishirini ya mtaji hisa wa Chama;

h) **"Hisa za hiari"** ni fedha ambayo mwanachama anaweka chamani na anaweza kuichukua wakati wowote anapoihitaji kwa mujibu wa sera;

i) **"Kanuni"** ina maana ya Kanuni za Vyama vya Ushirika;

j) **"Mfungamano wa Pamoja"** Wakulima, wafanyakazi, wafugaji na wajasiliamali.

k) **"Mrajis"** maana yake ni kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013;

l) **"Sera/Mwongozo**" maana yake ni utaratibu uliowekwa na wanachama kuongoza watendaji wa Chama katika uendeshaji wa shughuli za chama ili kufikia malengo yaliyowekwa kwa manufaa ya wanachama;

m) **"Sheria"** ina maana ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013;

n) **"Tume",** ina maana Tume ya Maendeleo ya Vyama vya

Ushirika, Tanzania

## SEHEMU YA PILI

## TAARIFA ZA CHAMA

| | | |
|---|---|---|
| Jina la chama | 3 | Jina la chama ni **Wakulima wa Mara Co-operative Union (WAMACU) Ltd.** |
| Anuani ya chama | 4 | (1) Anuani ya Chama ni S.L.P 228, Tarime, Mara. |
| | | (2) Mabadiliko yoyote ya anuani, eneo la Ofisi ya Chama yatapaswa yatolewe taarifa kwa maandishi kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika na mabadiliko hayo hayatasababisha marekebisho ya Masharti ya Chama. |
| Fungamano la Pamoja | 5 | **Fungamano** la pamoja katika Chama litakuwa ni wakulima, wafanyakazi, wafugaji, wavuvi, na wajasiliamali. |
| Eneo la shughuli za Chama | 6 | Eneo la shughuli za Chama litakuwa **TARIME.** |
| Tarehe ya kusajiliwa na namba ya Usajili | 7 | Chama kimesajiliwa tarehe **24/12/2008** na kupewa Hati Na **5573** |
| Mwaka wa fedha | 8 | Mwaka wa fedha wa Chama utakuwa ni kipindi cha miezi kumi na miwili kuanzia tarehe 1 **April** na kukomea tarehe 31 |

ya mwezi **Machi ya mwaka unaofuata.**

## SEHEMU YA TATU

## MADHUMUNI

Madhumuni ya Chama

9 Madhumuni ya kuanzishwa kwa Chama ni kuinua, kuimarisha na kuendeleza hali ya kiuchumi na kijamii ya wanachama wake kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu za Vyama vya Ushirika. Ili kufikia madhumuni haya, Chama kitafanya yafuatayo: -

a) Kukusanya, kuhifadhi, kusindika, na kuuza mazao ya vyama wanachama kwa kuzingati kanuni za Vyama vya Ushirika vya mwaka 2015;

b) Kununua, kuuza, kuhifadhi, kusambaza, na kuuza zana na pembejeo za kilimo kwa wanachama wake;

c) Kuwakopesha wanachama wake fedha kwa ajili ya kukusanyia mazao;

d) Kukopa toka taasisi zinazokopesha fedha kwa ajili ya kukusanyia mazao;

e) Kusimamia, kuratibu na kusafirisha mazao ya wanachama wake kwenda viwandani na kwenye masoko;

f) Kuanzisha na kuimarisha viwanda vya kusindika na

kuongeza thamani kwa mazao, na hatimaye kuyauza kwa tija;

g) Kupokea na kuweka amana za wanachama;

h) Kutoa huduma zinazohusu utunzaji wa Vitabu vya Mahesabu;

i) Kutoa elimu ya ushirika kwa wanachama, viongozi na watendaji;

j) Kuhimiza wanachama wake kufanya maandalizi ya makisio ya mapato na matumizi na kuyapeleka kwa Mrajisi wa Vyama vya Ushirika kwa ajili ya kuidhinishwa;

k) Chama kinaweza kuungana na Vyama Vikuu vingine na kuunda/kujiunga na shirikisho;

l) Kufanya mambo mengine yote yanayohusu maendeleo ya chama na wanachama wake kulingana na sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013 na kanuni zake za mwaka 2015.

m) Kuunganisha nguvu na jitihada za wanachama katika kuandaa miradi ya Chama na kutafuta masoko ya bidhaa na fedha zinazozalishwa;

n) Kutathimini maendeleo yaliyopatikana ili kuboresha wanachama wengine, pamoja na kubuni miradi

itakayosaidia kujiimarisha kifedha;

o) Kujishughulisha na maswala ya mtambuka ya maendeleo ya jamii ikiwemo ukimwi, COVID19 na magonjwa mlipuko mengineyo, mazingira na jinsia;

p) Kupokea na kutunza Akiba na Amana za wanachama kwa njia rahisi na salama huku ikilipa riba kadri wanachama watakavyokubaliana;

q) Kutafuta vyanzo vya fedha ili kujenga na kuimarisha mtaji kwa ajili ya kutoa huduma kwa wanachama kwa masharti nafuu;

r) Kuwaelimisha wanachama kujijengea tabia ya kukopa kwa busara na kutumia vizuri mikopo kwa ajili ya kukusanyia mazao na kuinua hali zao za maisha kiuchumi na kijamii;

s) Kubuni na kutoa bidhaa mbalimbali za kifedha kwa wanachama ili waweze kushiriki zaidi katika kuimarisha mtaji wa Chama na mitaji yao binafsi na kuleta mvuto kwa wasio wanachama kujiunga na chama;

t) Kuweka kwa usalama fedha za chama na wanachama kwa kuanzisha mipango ya kukabiliana na majanga na/au kuweka bima za fedha zinazofaa;

u) Kuwashauri wanachama kuandaa mipango yao ya maendeleo katika kuwekeza mitaji kwenye miradi ya kiuchumi na huduma za jamii;

v) Kutoa elimu na mafunzo mbalimbali kwa wanachama, Bodi na watendaji ili kuendana na kasi ya ushindani katika biashara ya mazao.

w) Kutoa elimu kwa wanachama kuhusu dhana ya Ushirika, Elimu ya Fedha na manufaa yake, Ujasiriamali katika mazao na tasnia nyingine zinazohusiana na miradi inayoendeshwa na kutekelezwa na wanachama wake.

x) Kuwekeza katika taasisi za kifedha, hisa na dhamana kwenye vyombo vya Fedha, Serikali na Taasisi zingine kwa manufaa ya Chama na Wanachama wake.

y) Kufanya mambo mengine ambayo yataimarisha na kuendeleza hali ya uchumi wa chama na wanachama.

z) Kuwekeza katika miradi ya kilimo, mazingira, uchakataji na uongezaji thamani ya mazao ghafi na hatimaye kuuza kwa tija, usafi pamoja na maswala yote yanayohusu kilimo, uvuvi, mifugo na ujasiliamali;

aa) Kuweka mfumo wa thabiti wa TEHAMA katika shughuli zote zinazoendeshwa na chama.

## SEHEMU YA NNE

## UANACHAMA

Sifa za uanachama

10 Chama/Taasisi/ (Mtu Binafsi) yoyote anaweza kujiunga na chama endapo atakidhi mahitaji ya Fungamano la pamoja la uanachama na sharti awe na sifa zifuatazo; -

a) Kiwe chama cha ushirika cha msingi cha mazao kilichosajiliwa na kinafanya shughuli zake katika eneo la Chama;

b) Kiwe kimelipa kiingilio, hisa na michango kwa mujibu wa mashariti haya;

c) Kiwe tayari kufuata mashariti, kanuni na sheria ya Vyama vya Ushirika;

d) Kiwe kimelipa kiingilio cha **Tshs.50,000/=**, hisa za uanachama ambapo moja ni **Tshs. 200,000/=** na kuweka akiba kwa kiwango kilichowekwa kwa mujibu wa masharti haya na kiwe tayari kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za chama.

e) Hisa iwe 200,000/= lakini ilipwendani ya mwaka mzima, na mafungu yote yakamilishwe nadani ya

miaka mitano (5).

f) Fedha ya hisa ifunguliwe akaunti ya Hisa ili kuepuka kutumia hisa za wanachama.s

g) Kiwe chama kinachoelewa na kuwa tayari kutekeleza madhumuni ya Chama Kikuu kama yalivyoainishwa kwenye masharti haya na kufafanuliwa katika nyaraka mbalimbali.

h) **Kikundi: -**

  (i) Kiwe ni chama au ushirika uliosajiliwa kisheria na kufanya shughuli zake katika kanda ya ziwa Mashariki na shughuli zake kulandana na za chama husika;

  (ii) Kiwe kimefanya shughuli zake si chini ya miaka miwili;

  (iii) Kiwe kimelipa kingilio cta Tshs. 50,000/= na hisa ya Tshs. 50,000/= kwa mujibu wa mashariti ya Chama cha Ushirika cha WAMACU LTD;

  (iv) Kiwe kimeweka akiba na amana na kiwe kinashiriki shughuli zote za Chama Kikuu kikamilifu;

  (v) Kikundi au Ushirika kitateua mjumbe mmoja

atakaye kuwa mwakilishi wake katika shughuli za Chama.

Wanachama

11 Wanachama wa Chama Kikuu cha WAMACU LTD watatokana na: -

a) Vyama vyote vilivyoshiriki katika mchakato wa uanzilishi na kuomba kuandikishwa kwa Chama Kikuu na ambavyo vimetimiza masharti ya uanachama kwa mujibu wa Masharti haya; na

b) Vyama vingine vyote vya ushirika vya mazao/taasisi/mtu binafsi vitakavyojiunga na Chama Kikuu baada ya kukubaliwa na Bodi na kupitishwa na Mkutano Mkuu.

Taratibu za kujiunga na chama

12 Maombi ya kujiunga katika Chama Kikuu yatafuata utaratibu ufuatao: -

a) Chama/Taasisi/Mtu chochote kitakachokuwa kimetimiza sharti **Na.10** kitaomba uanachama kwa kujaza fomu iliyoandaliwa na Chama Kikuu.

b) Mwombaji atajadiliwa na bodi ili kujiridhisha iwapo inakidhi vigezo vya kuwa mwanachama na Bodi inaweza kumkubali au kumkataa.

c) Pendekezo la Bodi ya Uongozi litapelekwa mbele ya

Mkutano Mkuu kwa uthibitisho ambapo waombaji wote waliokubaliwa na Bodi wanayo haki ya kuhudhuria Mkutano Mkuu huo na kujadiliwa na wajumbe wa Mkutano Mkuu na uamuzi wa Mkutano Mkuu utakuwa wa mwisho;

d) Mwombaji atakapokubaliwa na Bodi atatakiwa kulipa Kiingilio na Hisa na baada ya kupokelewa na Mkutano Mkuu atatakiwa kutia saini yake au kuweka dole gumba katika daftari la wanachama mbele ya wajumbe wa Bodi wawili;

e) Mwanachama akishapitishwa na Mkutano Mkuu atakuwa na haki ya kupatiwa kitambulisho cha uanachama (Hati ya Hisa) na endapo kitambulisho kitapotea, mwanachama atapewa kitambulisho kingine kwa kulipa gharama kwa kuzingatia kiwango kitachachowekwa na Bodi na kuidhinishwa na Mkutano Mkuu.

Taarifa ya kukataliwa uanachama

13 Endapo maombi ya kujiunga na chama yatakataliwa na Bodi ya Uongozi: -

a) Bodi ya Uongozi itapaswa kumwandikia mwombaji barua ya kumjulisha kuhusu kukataliwa kwa maombi yake ikieleza sababu za kukataliwa.

b) Mwombaji ambaye maombi yake yatakataliwa na Bodi ya Uongozi anaweza kukata rufaa kwa maandishi kwa Mkutano Mkuu kupitia kwa Afisa Ushirika wa eneo husika ambaye ataiwasilisha kwenye Mkutano Mkuu ambao utatoa uamuzi wa mwisho.

Kiingilio, Hisa na Akiba

14 (1) Mwanachama atakapokubali kujiunga na Chama atapaswa: -

a) Kulipa kiingilio cha shilingi Tshs. 50,000/=

b) Kununua idadi ya hisa tano zenye thamani ya shilingi milioni moja (1,000,000/=) kwa kila hisa 200,000/= na ili awe mwanachama atapaswa kununua na kulipia kikamilifu angalau 20% ya hisa na hisa zilizobaki atapaswa kuzilipia katika kipindi cha miaka mitano (5)

c) Kuweka Akiba kwa hiari yake kwa ajili ya maendeleo yake na pia anaweza kuitumia kama dhamana ya mkopo kwenye Chama Kikuu.

(2) Mwanachama ambaye atashindwa kutimiza matakwa ya sharti dogo (1) (b) hapo juu hataruhusiwa kunufaika na haki za mwanachama katika chama.

(3) Viwango vya kiingilio, hisa na akiba vinaweza kubadilishwa kwa maamuzi ya Mkutano Mkuu.

(4) Mwanachama aliyekamilisha kulipia Hisa zote atapewa hati ya kumiliki Hisa, (shares certificate)

Kuteua Mrithi

15 (1) ikiwa mwanachama ni mtu binafsi atamteua mrithi wake ambaye atakuwa na haki ya kulipwa hisa au maslahi mengine katika Chama.

(2) Mwanachama atakuwa na haki ya kubadilisha jina la mrithi.

(3) Kila uteuzi wa mrithi utaandikwa katika daftari la wanachama na utatiwa saini na mwanachama.

Kukoma uanachama

16 Uanachama utakoma: -

a) Iwapo Chama cha msingi cha mazao hakifuati na kutii mashariti, maadili, na miiko ya Chama Kikuu;
b) Iwapo Chama cha Msingi cha mazao hakiheshimu na hakitekelezi ahadi kinachotoa mfano kutotimiza makisio; kutotoa taarifa ipasavyo na kutotoa ushirikiano kwa Chama Kikuu katika mambo mbalimbali;
c) Iwapo chama cha msingi kitakuwa na mwenendo mbaya na kujihusisha na vitendo vya kuangusha na kuharibu sifa njema ya Chama Kikuu;
d) Kujiuzulu baada ya kutoa taarifa ya maandishi kwa

Bodi ya chama.

e) Kufukuzwa na wanachama katika Mkutano Mkuu kwa idadi ya wanachama wasiopungua nusu (1/2) ya waliohudhuria na kupiga kura baada ya kupewa nafasi ya kujitetea;

f) Kutenda kosa lolote ambalo limetajwa katika Sheria ya Vyama vya Ushirika, Kanuni na Masharti ya Chama;

g) Kutomiliki Hisa kwa mujibu wa masharti haya;

h) Kutohudhuria Mikutano Mikuu mitatu mfululizo pasipo kutoa taarifa ya maandishi kwa uongozi kwa njia inayokubalika na chama;

i) Kutoa au kupokea rushwa kwa nia ya kupata upendeleo;

Malipo na haki za mwanachama aliyejitoa au kufukuzwa uanachama

17 Mwanachama aliyejitoa au kufukuzwa uanachama atalipwa haki zake zote ndani ya kipindi cha miezi tatu kuanzia siku ya kukoma uanachama.

Kusimamishwa na kufutiwa uanachama

18 (1) Mwanachama anaweza kusimamishwa uanachama kutokana na sababu zifuatazo: -

a) Kutotekeleza ahadi alizotoa katika chama;

b) Kutotekeleza maazimio yaliyotolewa na kukubaliwa katika Mkutano Mkuu;

c) Kutoshiriki katika shughuli za kiuchumi za Chama Kikuu kwa muda wa miezi 6 mfululizo;

d) Kama itakavyoelekezwa kwenye Sheria ya Vyama vya Ushirika pamoja na Kanuni zake.

(2) Kabla ya kumsimamisha mwanachama husika, Bodi ya Chama itapaswa kumwandikia mhusika Notisi ya kusudio la kumsimamisha uanachama ikieleza sababu ya kusudio hilo na kumtaka kutoa maelezo ndani ya muda wa siku thelathini kueleza kwanini kusudio hilo lisitekelezwe.

(3) Iwapo Bodi ya Uongozi itaazimia kumsimamisha mwanachama itamwelekeza Meneja/Katibu wa chama kumwandikia mwanachama husika barua ya kumtaarifu kuhusu kusimamishwa kwake kusubiri maamuzi ya Mkutano Mkuu.

(4) Bodi ya Uongozi itawasilisha taarifa ya kusimamishwa uanachama kwenye Mkutano Mkuu pamoja na mapendekezo yake na Mkutano Mkuu, utapaswa kujadili na kutoa maamuzi ya kusimamishwa, kufutiwa

uanachama au kubatilisha maamuzi ya Bodi.

(5) Baada ya uamuzi wa Mkutano Mkuu Bodi ya Uongozi itapaswa kumjulisha mwanachama husika kwa maandishi kuhusu maamuzi hayo katika muda usiozidi siku saba tangu tarehe ya maamuzi.

(6) Mwanachama ambaye hataridhika na maamuzi ya Mkutano Mkuu atakuwa na haki ya kukata rufaa kwa Tume ndani ya muda wa siku thelathini tangu tarehe ya kupokea taarifa ya maamuzi ya Mkutano Mkuu.

Kupokelewa tena kwenye chama

19 Mwanachama aliyejiuzulu/aliyefukuzwa anaweza kukubaliwa na kupokelewa tena kujiunga na chama baada ya kutuma maombi kwa kufuata masharti haya na baada ya kulipa madeni yote aliyokuwa anadaiwa wakati anakoma kuwa mwanachama

Wajibu wa Mwanachama

20 Wajibu wa mwanachama utakuwa ni pamoja na: -

a) Kukamilisha kununua hisa na kulipa michango kama itakavyoagizwa na Mkutano Mkuu kwa kuzingatia Masharti ya Chama;

b) Kuendelea kununua hisa Zaidi ili kuongeza mtaji wa chama

c) Kufuata na kutekeleza Sheria ya Vyama vya Ushirika na

Kanuni zake, Masharti ya chama, maamuzi ya Mkutano Mkuu na maelekezo mengine halali kwa mujibu wa Sheria za nchi;

d) Kuwa mwaminifu kwa kushiriki kikamilifu katika shughuli za chama ili kutimiza madhumuni yake;

e) Kutoa michango mbalimbali katika kuendeleza madhumuni ya chama kadri itakavyoamuriwa na Mkutano Mkuu;

f) Kubeba dhamana endapo janga lolote litakipata chama;

g) Kuwa mwaminifu na kuonesha ushirikiano katika kutekeleza shughuli za chama;

h) Kudhamini mkopo wa Chama Kikuu na haki ya kudhaminiwa na mwanachama uliyemdhamini katika kipindi kile kile;

i) Kulipa mkopo alioudhamini endapo mdhaminiwa/mkopaji atashindwa kulipa mkopo wake; na

j) Kuhudhuria semina na mafunzo yanayotolewa na Chama.

k) Kuhudhuria mikutano yote inayomhusu kwa mujibu wa

masharriti.

Haki za Mwanachama

21 Mwanachama atakuwa na haki zifuatazo:

i) Kushiriki kikamilifu katika shughuli za Chama ikiwa ni pamoja na kuhudhuria mikutano yote inayohusika;

ii) Kila chama mwanachama atakuwa na haki ya kuchagua wajumbe watakao kiwakilisha chama katika Mkutano Mkuu kwa mujibu wa kanuni ya 33(2) ya mwaka 2015;

iii) Kati ya wajumbe wawili mmoja sharti atoke ndani ya Bodi ya chama cha msingi na mmoja atoke nje ya BODI;

iv) Kushiriki katika kutoa uamuzi wa mambo mbalimbali katika Mikutano Mikuu;

v) Kupiga kura chini ya misingi ya mtu mmoja kura moja bila kujali idadi ya Hisa anazomiliki;

vi) Kuchagua na/au kuchaguliwa katika Uongozi wa chama.

vii) Kuwa na haki sawa kuhusu mali ya Chama na kudhibiti ipasavyo matumizi yake;

viii) Kupatiwa huduma zozote zinazotolewa na chama ili mradi amekidhi masharti yanayoambatana na huduma

hiyo;

ix) Kupatiwa taarifa mbalimbali za shughuli za chama, muhtasari wa mkutano na nyaraka nyingine za chama kwa ajili ya mapitio akiwa katika ofisi za chama;

x) Kuitisha Mkutano Mkuu kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika na Kanuni zake pamoja na masharti haya;

xi) Kuteua Mrithi;

xii) Kukata rufaa dhidi ya maamuzi ya Bodi ya Uongozi na Mkutano Mkuu;

xiii) Kuona na kusoma mashariti mizania, nyaraka za Mrajisi, na mihtasari ya Mikutano Mikuu wakati wa saa za kazi;

xiv) Kupokea gawio na faida nyingine kutoka katika shughuli za chama kwa kuzingatia masharti; na

xv) Kupewa kitabu cha Hati ya Hisa au kifaa kingine chenye makusudi hayo.

Matumizi ya Stahili za mwanachama aliyekoma kuwa

22 Stahiki za mwanachama aliyekoma uanachama kutokana na sababu zilizotajwa katika kipengele namba 18 cha masharti haya, zinaweza kutumika kama ifuatavyo: -

mwanachama

i) Kulipia mikopo na gharama zingine ambazo mwanachama anadaiwa na Chama;

ii) Bakaa kulipwa kwa mwanachama mwenyewe au kwa mrithi wake aliyeainishwa katika daftari la wanachama; na

iii) Iwapo mwanachama huyo hajulikani alipo na hakuna mrithi au mwakilishi wa kisheria wa mwanachama huyo bakaa ya maslahi yake yatatumika kwa mujibu wa kanuni ya 37 (6) ya Kanuni za Vyama vya Ushirika.

Dhima ya mwanachama

23 Dhima ya mwanachama kwa madeni ya chama itakuwa ni ya ukomo wa kiwango cha thamani ya Hisa zake ambazo zimelipwa na hazijalipwa.

## SEHEMU YA TANO

## FEDHA NA MALI ZA CHAMA

Vyanzo vya fedha

24 Fedha kwenye chama zitatokana na: -

a) Viingilio, ada, mauzo ya masharti na fomu mbalimbali na michango maalum kutoka kwa wanachama;

b) Ushuru wa mazao;

c) Hisa za uanachama;

d) Riba juu ya mikopo vyama wanachama;

e) Mikopo itakayotoka benki, asasi nyingine za fedha na mifuko ya hifadhi za jamii kwa kuzingatia sheria.

f) Misaada na ruzuku kutoka kwa watu binafsi, taasisi na asasi nyingine;

g) Ziada halisi ya Chama;

h) Ziada itokanayo na miradi mingine ya chama kama vile miradi ya kilimo na mifugo, mazingira, biashara ya madini na usafi;

i) Fedha za akiba ya lazima na malimbikizo;

j) Akiba, hisa za hiari na amana za wanachama kwa AMCOS zinazohusika.

k) Mapato mengineyo halali.

Mali za Chama

25 Mali za Chama zitakuwa ni pamoja na:-

a) Fedha taslimu mkononi na fedha zilizopo Benki;

b) Bakaa ya mazao ghalani ya vyama wanachama na wadaiwa wengine.

c) Uwekezaji katika taasisi mbalimbali;

d) Mifumo laini na mali zisizoshikika;

e) Vifaa, mitambo, mashine na zana zote za chama; na

f) Majengo na mali nyingine za chama kama zitakavyooneshwa kwenye daftari la mali za chama.

Mali za Chama kuwekwa Rehani

26 Mali za Chama zitawekwa rehani kwa idhini ya Mkutano Mkuu na kuidhinishwa na Mrajis kwa kuzingatia Sheria zilizopo.

Ukaguzi wa Hesabu za chama

27 Kila mwisho wa mwaka wa fedha hesabu za chama zitakaguliwa na Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) au kampuni au mkaguzi mwingine atakayependekezwa na wanachama na kuidhinishwa na Mrajis.

## SEHEMU YA SITA:

## TARATIBU KUHUSU HISA, AKIBA, NA AMANA.

Uwekaji Hisa, Akiba, na Amana

28 (1) Kila mwanachama atatakiwa kuweka Akiba katika kila kipindi kilichokubalika ya kiasi kisichopungua shilingi laki moja au kiasi kingine kadiri itakavyoamuliwa na Mkutano Mkuu.

(2) Chama kinaweza kupokea Hisa za Hiari kutoka kwa wanachama

(3) Akiba ya mwanachama na Hisa za Hiari zinaweza kutumika kama dhamana ya mkopo katika taasisi za fedha.

(4) Akiba, Hisa za Hiari na Amana za wanachama zitatunzwa au kuwekezwa katika sehemu ya usalama

kama ilivyoelekezwa na sheria, kanuni na sera inayohusika na sehemu kubwa zitawekwa benki

(5) Mwanachama anaweza kupunguza Akiba yake kwa kufuata taratibu zilizowekwa na Chama kwenye Sera husika.

(6) Faida juu ya Akiba zitalipwa kwa kiwango kilichoainishwa kwenye Sera husika au kiwango kingine kitakachopitishwa na Mkutano Mkuu.

Utunzaji wa kitabu au taarifa za mwanachama

29 (1) Kila mwanachama atapewa kitabu/cheti cha Hisa cha Akiba (share certificate) kilicho katika nakala ngumu au laini ambacho kitafanyiwa maingizo ya miamala mbalimbali inayomhusu mwanachama.

(2) Kitabu/Hati ya Hisa ni mali ya mwanachama, atatakiwa kukionesha wakati wowote anapofanya muamala ya chama cha msingi.

(3) Endapo mwanachama atapoteza Hati ya Hisa, anatakiwa kutoa taarifa kwenye chama na kupatiwa hati nyingine kwa kulipia kiasi cha shilingi 10,000/= au kiasi kingine kitakachoidhinishwa na Mkutano Mkuu.

(4) Mwanachama anatakiwa kutunza hati yake na haruhusiwi kufanya maingizo ya muamala wowote

mwenyewe.

(5) Endapo mwanachama atafanya maingizo ya muamala wowote mwenyewe atakuwa ametenda kosa la jinai na atapaswa kushtakiwa kwa mujibu wa Sheria ya Makosa ya Jinai.

## SEHEMU YA SABA

## UHIFADHI WA FEDHA ZA CHAMA

Uhifadhi wa fedha za chama

30 (1) Fedha za chama zitahifadhiwa katika taasisi za fedha.

(2) Kanuni za Fedha za chama zitaainisha kiwango cha fedha ambacho kinaweza kuchukuliwa kutoka benki na kutunzwa kwenye ofisi za chama kama fedha kichele.

(3) Fedha za chama zitapokelewa kwa mlipaji kuwasilisha risiti halisi ya malipo ya benki au kwa njia ya mitandao ya simu au kuwasilisha fedha taslimu ofisini kulingana na taratibu zilizoainishwa katika kanuni za fedha.

(4) Malipo yote ya kawaida na yanayozidi 1,000,000/= yatafanywa kwa njia ya hundi, hamisho la benki na kupitia katika mitandao ya simu.

(5) Fedha za chama zitatumika kwa madhumuni makuu yafuatayo: -

a) Kukusanya, kuhifadhi, kusindika, na kuuza mazao yanayoshughulikiwa na chama;
b) Kununua zana za kilimo na pembejeo

zinazohitajika kuendeleza chama; na

c) Malipo kwa uendeshaji shughuli za chama.

## SEHEMU YA NANE

## MATENGO NA MGAO WA ZIADA

Mfuko wa Matengo ya Kisheria

31 Matengo ya mfuko wa kisheria na matumizi yake yatafanywa kwa kuzingatia Kanuni ya 68 ya Kanuni za Vyama vya Ushirika.

Mfuko wa Elimu na mafunzo

32 Matengo ya mfuko wa elimu na mafunzo pamoja na matumizi yake yatafanywa kwa mujibu wa Kanuni ya Vyama vya Ushirika Na. 69 ya mwaka 2015.

Mgao wa ziada halisi

33 (1) Ziada halisi ya mwaka iliyopatikana mara baada ya kukaguliwa na mkaguzi aliyeidhinishwa, kitatumika mara baada ya kukidhi matakwa ya Kanuni ya mwaka 2015

(2) Bila kuathiri sharti la 33(1), mgawanyo wa ziada halisi utakuwa kama ifuatavyo; -

(a) Asilimia isiyopungua ishirini (20%) ya malimbikizo ya ziada kwa mwaka zitapaswa kutengwa na kuwekwa katika Fungu la Akiba ya Lazima kwa ajili ya kuendeleza chama;

(b) Kiwango kisichopungua asilimia kumi na tano (15%) kitatengwa kwa ajili ya kukombolea madeni mabaya na

yenye mashaka;

(c) Asilimia kumi na tano (15%) itatengwa kwa ajili ya Mfuko wa Kukombolea Hisa na,

(d) Bakaa ya ziada halisi ya mwaka inaweza kugawanywa kama itakavyoamuliwa na Mkutano Mkuu na kuidhinishwa na Mrajis kwa ajili ya shughuli zifuatazo: -

i) Kwa ajili ya kulipia faida juu ya Hisa;

ii) Gawio la ziada kwa wanachama;

iii) Zawadi kwa Bodi na watumishi wa kujitolea;

iv) Kuchangia mifuko ya maendeleo kama itakuwepo;

v) Kuchangia shughuli za hisani katika jamii; na

vi) Mambo mengine kama itakavyoamuliwa na Mkutano Mkuu kwa kuzingatia kifungu cha 79 cha Sheria ya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013.

(3) Kwa madhumuni ya kutekeleza Aya ya (v) ya sharti dogo la (d) (i) hapo juu chama kitaanzisha na kutunisha Mfuko Maalumu kwa ajili ya kuchangia shughuli za hisani; pia kwa madhumuni ya Akaunti maalum kwa ajili ya kuweka Fedha za matengo.

## SEHEMU YA TISA

## USIMAMIZI NA UONGOZI WA CHAMA

Mamlaka ya Mkutano Mkuu

34 (1) Mkutano Mkuu wa wanachama utakuwa na mamlaka ya juu katika kuamua, kuongoza na kusimamia shughuli zote za maendeleo ya chama.

(2) Madaraka ya juu ya chama yatakuwa mikononi mwa wanachama waliohudhuria na kupiga kura katika Mikutano Mikuu.

(3) Kutakuwa na aina tatu za Mikutano Mikuu ambayo ni mkutano Mkuu wa Mwaka, Mkutano Mkuu wa Kawaida na Mkutano Mkuu Maalum.

Mkutano Mkuu wa Mwaka

35 (1) Mkutano Mkuu wa Mwaka utapaswa kufanyika ndani ya miezi tisa baada ya kufungwa kwa mwaka wa fedha wa chama uliotangulia.

(2) Kwa kuzingatia Kanuni za Vyama vya Ushirika, masuala yatakayofanyika katika Mkutano Mkuu wa Mwaka ni pamoja na: -

a) Kusoma, kujadili na kuthibitisha muhtasari wa Mkutano Mkuu uliopita;

b) Yatokanayo na muhtasari wa Mkutano Mkuu uliopita;

c) Kupokea na kujadili taarifa ya mwaka ya Bodi;

d) Kupokea na kujadili wanachama wapya, waliojitoa, au waliosimamishwa uanachama;

e) Kupokea na kujadili hesabu zilizokaguliwa, taarifa ya ukaguzi Menejimenti pamoja na taarifa ya ukaguzi ya Mrajis;

f) Kujadili namna ya kugawa ziada kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika, 2013 na Kanuni zake pamoja na Masharti haya;

g) Kujadili na kuidhinisha mpango mkakati, mpango wa biashara wa chama na program ya utekelezaji na kutathimini utekelezaji wake;

h) Kuweka na kuidhinisha viwango vya ada na michango mbalimbali;

i) Kuteua Mkaguzi wa Nje kwa ajili ya ukaguzi wa hesabu za chama kwa mwaka unaofuata;

j) Kujadili na kupitisha kiwango cha zawadi (Honoraria) kwa Bodi na watumishi wanaojitolea kadiri itakavyoonekana inafaa;

k) Kujadili na kuidhinisha bajeti ya mapato na matumizi ya Chama kwa mwaka unaofuata, na kuiwasilisha kwa Mrajis kwa ajili ya kuidhinishwa;

l) Kujadili na kuweka ukomo wa madeni kwa mwaka unaofuata;

m) Kufanya uchaguzi wa wajumbe wa Bodi na kuwasimamisha na kuwafukuza ikibidi;

n) Kuidhinisha ununuzi au uuzaji wa mali za chama zinazozidi shilingi milioni ishirini (20,000,000/=)

o) Kufanya marekebisho ya masharti ya Chama inapobidi;

p) Kujadili na kuamua juu ya mapendekezo ya sera, miongozo na kanuni mbalimbali za chama;

q) Kupokea na kujadili jambo lolote litakaloletwa na Bodi mbele ya Mkutano Mkuu kwa maendeleo ya Chama;

r) Kujadili na kuidhinisha mipango ya uwekezaji ya Chama;

s) Kujadili na kuazimia rufaa za wanachama;

t) Kujadili na kuidhinisha uombaji wa leseni ya kuuza mazo ya kahawa nje kutoka BODI YA KAHAWA, na

u) Kujadili mambo mengineyo yote yahusuyo maendeleo ya chama.

Mkutano Mkuu wa Kawaida

36 (1) Chama kinaweza kufanya Mkutano Mkuu wa Kawaida angalau mara moja kwa mwaka.

(2) Mambo yatakayozungumzwa katika Mkutano Mkuu wa Kawaida ni pamoja na: -

a) Kusoma na kuthibitisha mambo ya mkutano uliopita;

b) Kujadili na kuidhinisha ununuzi au uuzaji wa mali ya chama inayohamishika au isiyohamishika inayozidi thamani ya shilingi milioni ishirini 20,000,000/=

c) Kufanya marekebisho ya Masharti inapoonekana haja ya kufanya hivyo;

d) Kuidhinisha makisio ya mapato na matumizi ya chama;

e) Kuweka ukomo wa madeni;

f) Kupitia taarifa ya utendaji wa Bodi;

g) Kuidhinisha mikataba ya Chama;

h) Kuweka na kuidhinisha idadi ya Wajumbe wa Bodi;

i) Kutafakari namna ya kuitekeleza Sera ya Maendeleo ya Ushirika;

j) Kujadili na kuidhinisha mikataba inayoingiwa na chama;

k) Kuthibitisha wanachama wapya na kuchukua hatua za

kinidhamu kwa wanachama wakorofi;

l) Kuchagua au kuwafukuza Wajumbe wa Bodi;

m) Kuchagua wajumbe wa kukiwakilisha chama katika vyama na Taasisi nyingine zinazohusika na maendeleo ya chama;

n) Kujadili na kupitisha utaratibu wa kazi na kutathmini shughuli za utendaji ili kuleta ufanisi;

o) Kujadili na kutathimini uwezekano wa kuomba leseni ya Direct Export;

p) Kujadili mambo mengineyo yanayohusu maendeleo ya Chama.

(3) Bila kujali matakwa ya sharti dogo (1) mambo ya Mkutano Mkuu wa Kawaida yanaweza kujumuishwa na kujadiliwa pamoja na mambo ya Mkutano Mkuu wa Mwaka katika Mkutano Mkuu wa Mwaka.

Mkutano Mkuu Maalumu

37 (1) Kutakuwepo na Mkutano Mkuu Maalum wakati wowote unapohitajika ambao unaweza kuitishwa na: -

a) Mrajis wa Vyama vya Ushirika au Afisa yeyote aliyeidhinishwa naye;

b) Wanachama; kwa maombi ya maandishi ya wanachama

wasiopungua moja ya tatu (1/3) ya wanachama wote ambayo yatapaswa yafafanue jambo litakalozungumzwa, yawekwe saini au alama ya dole gumba na waombaji, yaambatishwe na nakala za vitambulisho vya waombaji na nakala ya maombi hayo na kutumwa kwa mamlaka husika.

c) Wajumbe wa Bodi ya Uongozi.

(2) Mkutano Mkuu Maalumu utakaoitishwa na wanachama au Bodi ya Chama utakuwa na agenda moja tu.

(3) Mkutano Mkuu Maalumu utakaoitishwa na Mrajis au Afisa aliyeidhinishwa naye utaongozwa na Mrajis mwenyewe au mwakilishi wake na utaelekeza mambo atakayoyawasilisha.

Notisi ya Mkutano Mkuu

38 (1) Notisi ya Mkutano Mkuu lazima ioneshe bayana tarehe, saa na mahali pa kufanyia mkutano pamoja na mambo yatakayojadiliwa na itapaswa kubandikwa katika ofisi ya Chama na kwenye mbao za matangazo.

(2) Bodi ya Uongozi inaweza kutumia njia nyingine za mawasiliano kama simu, barua pepe, Runinga au matangazo ya redio katika kuhakikisha notisi ya Mkutano Mkuu inawafikia wajumbe wa Mkutano Mkuu kwa wakati.

(3) Muda wa notisi ya Mkutano Mkuu utakuwa: -

i) Kwa Mkutano Mkuu wa Mwaka na Mkutano Mkuu wa Kawaida siyo chini ya siku ishirini na moja (21) kabla ya tarehe ya kufanyika mkutano;

iii) Kwa Mkutano Mkuu Maalum notisi haitakuwa chini ya siku saba (7).

(ii) Notisi itakayotolewa kwa mujibu wa aya za (i) na (ii) hapo juu itapaswa kuambatanishwa na ajenda za mkutano na nyaraka au makabrasha yenye taarifa zitakazojadiliwa katika mkutano huo.

Akidi ya Mkutano Mkuu

39 (1) Akidi katika Mikutano Mikuu yote, isipokuwa Mkutano Mkuu Maalumu ulioitishwa na Mrajis, itakuwa si chini ya nusu (1/2) ya wanachama wote au wanachama mia moja (100) ikichukuliwa idadi yoyote iliyo ndogo.

(2) Ikiwa katika Mkutano Mkuu wa mwaka au katika Mikutano Mikuu ya kawaida akidi haijatimia baada ya kupita muda wa saa moja wa kusubiri tangu muda uliopangwa kuanza kwa Mkutano, Mwenyekiti wa Bodi ataahirisha mkutano huo kwa muda wa siku saba na utakapoitishwa tena masuala yatakayojadiliwa yatakuwa yale ya mkutano ulioahirishwa.

(3) Endapo Mkutano Mkuu ulioahirishwa umeitishwa baada

ya siku saba na akidi haikutimia baada ya kupita muda wa kusubiri uliopangwa kuanza mkutano, mkutano huo utafutwa na taarifa kupelekwa kwa Mrajis.

(4) Mkutano Mkuu Maalum ulioitishwa na Mrajis au mwakilishi wake utafanyika kwa muda uliopangwa hata kama akidi haijatimia na maazimio yatakayopitishwa katika mkutano huo yatakuwa halali.

Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu

40 Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu, isipokuwa Mkutano Mkuu Maalum ulioitishwa na Mrajis, atachaguliwa na wanachama katika kila Mkutano Mkuu na atahudumu kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 40 ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2015.

Upigaji kura katika Mkutano Mkuu

41 (1) Mwanachama yeyote ambaye ametimiza masharti ya uanachama kama ilivyo katika masharti haya atakuwa na kura moja katika Mkutano Mkuu wa chama na hakutakuwa na kura ya uwakilishi.

(2) Maazimio ya Mkutano Mkuu yatafanywa kwa kupiga kura ya kunyoosha mikono isipokuwa kama kura ya siri itahitajika na kuungwa mkono na wanachama wasiopungua nusu (1/2) ya wajumbe waliohudhuria kwenye Mkutano huo;

(3) Katika Mkutano Mkuu maamuzi ya wengi yatachukuliwa na endapo kura zitalingana jambo hilo litarudiwa kupigiwa

kura au kusubiri mkutano utakaofuata.

Muhtasari wa Mkutano Mkuu

42 (1) Kumbukumbu za masuala yote yaliyojadiliwa, kuamuliwa au kuazimiwa katika Mkutano Mkuu zitaandaliwa na kusainiwa na Katibu wa Mkutano na baada ya kuthibitishwa katika mkutano unaofuata kumbukumbu hizo zitasainiwa na Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu na kutunzwa katika kitabu cha kumbukumbu za mikutano.

(2) Bodi ya Uongozi ya Chama itapaswa kutuma nakala ya muhtasari uliyothibitishwa kwa Mrajis ndani ya siku thelathini tokea tarehe ya Mkutano Mkuu uliothibitisha muhtasari husika.

## SEHEMU YA KUMI

## BODI YA UONGOZI, KAMATI YA USIMAMIZI NA JIRA

Bodi ya Uongozi

43 (1) Kutakuwa na Bodi ya Uongozi ya Chama ambayo itakuwa na wajumbe wasiopungua watano (5) na wasiozidi tisa (9) akiwemo Mwenyekiti na Makamu wake; na watachaguliwa kutoka miongoni mwa wawakilishi wa vyama wanachama wa Mkutano Mkuu.

(2) Bila kuathiri matakwa ya sharti dogo la (1) Mkutano Mkuu unaweza kuweka idadi pungufu ya Wajumbe wa Bodi ya

Uongozi kwa kuzingatia mahitaji ya shughuli za chama kwa wakati uliopo.

(3) Wajumbe wa Bodi ya Uongozi ya Chama watachaguliwa na Mkutano Mkuu kwa kuzingatia kifungu cha 68 cha Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2013.

(4) Wajumbe wa Bodi ya Uongozi watahudumu katika nafasi hiyo kwa awamu moja ya kipindi cha miaka mitatu na wanaweza kuchaguliwa kuhudumu tena kwa awamu nyingine ya kipindi cha miaka mitatu na baada ya hapo hawataruhusiwa kugombea kwa awamu nyingine moja itakayofuatia.

(5) Mwenyekiti wa Bodi ya Uongozi na Makamu wake watachaguliwa na Mkutano Mkuu kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Bodi.

(6) Baada ya wajumbe wa bodi kuchaguliwa sharti wapate mafunzo yatakayowawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

(7) Kila mwisho wa mwaka wajumbe wa bodi wanapaswa kujaza fomu za kuainisha mali na Madeni waliyonayo. Mjumbe wa bodi ambae hatajaza fomu hizo atakuwa amekwenda kinyume cha maadili ya uongozi kulingana sheria Na. 6 ya vyama vya ushirika ya mwaka 2013.

Kukoma

44 Mjumbe wa Bodi ya Chama atakoma kuwa mjumbe,

Ujumbe wa Bodi;

endapo: -

a) Ameacha kuwa mwanachama wa chama cha msingi cha mazao;

b) Amepatwa na kichaa cha kudumu kilichothibitishwa na daktari wa hospitali inayotambulika kisheria;

c) Atatumia ofisi ya Chama Kikuu kwa manufaa yake binafsi;

d) Haheshimu maamuzi ya Bodi, au Mkutano Mkuu;

e) Anaingilia madaraka ya watendaji na kamati nyingine;

f) Hahofii miiko na maadili ya Chama

g) Kifo;

h) Kutochaguliwa tena na Mkutano Mkuu;

i) Atafanya shughuli zozote zinazofanana na shughuli zinazofanywa na Chama Kikuu.

j) Atafukuzwa na Mkutano Mkuu kwa azimio lililoungwa mkono na idadi ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wasiopungua nusu (1/2) ya wajumbe waliohudhuria kwenye Mkutano huo;

k) Kuacha kuwa mwakilishi wa chama mwanachama

kwenye Mkutano mkuu wa chama;

l) Kwa kushindwa kuhudhuria vikao vya Bodi vitatu mfululizo bila sababu za msingi; na

m) Kwa sababu nyingine zozote zilizoainishwa chini ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013 na Kanuni zake.

Vikao vya Bodi ya Uongozi

45 (1) Vikao vya Bodi ya Uongozi vitafanyika mara nne kwa mwaka na pale itakapohitajika Bodi inaweza kufanya vikao vya dharura viwili, Pamoja na vikao kazi visivyokuwa na malipo zaidi ya nauli na chakula.

(2) Bodi ya Uongozi itapaswa kuandaa ratiba ya vikao vya Bodi na kuiwasilisha kwa Mrajis na Mrajis Msaidizi wa Mkoa.

(3) Mwenyekiti wa Bodi ataongoza kikao cha Bodi na endapo hatakuwepo, Makamu Mwenyekiti ataongoza kikao hicho na iwapo wote wawili hawatakuwepo katika kikao hicho, mjumbe wa Bodi mwingine yeyote kati ya waliohudhuria atachaguliwa kuwa Mwenyekiti wa muda na ataongoza kikao hicho.

(4) Vikao vya Bodi vitakuwa halali iwapo wajumbe waliohudhuria watakuwa nusu ya wajumbe wote.

(5) Bodi inaweza kutumia njia za kisasa kama vile

kukutana kwa njia ya elektroniki (video conference, etc.) kukutana kufikia maamuzi. Vikao vyake vitafanyika katika ofisi za chama kikuu cha WAMACU LTD.

(5) Kila mjumbe wa Bodi atakuwa na kura moja na iwapo kura zitalingana, Mwenyekiti atakuwa na kura ya ziada.

Muhtasari wa Vikao vya Bodi ya Uongozi

46 Kumbukumbu za masuala yote yaliyojadiliwa, kuamuliwa au kuazimiwa katika vikao vya Bodi zitaandaliwa na kusainiwa na katibu na baada ya kuthibitishwa katika kikao kinachofuata, kumbukumbu hizo zitasainiwa na Mwenyekiti wa Bodi na kutunzwa katika kitabu cha kumbukumbu za vikao vya Bodi.

Kazi za Bodi ya Uongozi

47 (1) Kwa kuzingatia Kanuni za vyama vya ushirika, Bodi ya Uongozi itakuwa na wajibu wa kusimamia shughuli za kila siku za chama.

(2) Bila kuathiri matakwa ya sharti dogo (1) Bodi ya chama itapaswa kutekeleza kazi zifuatazo: -

i) Kusimamia shughuli zote za Chama Kikuu na kuhakikisha kuwa zinaendeshwa ipasavyo;

ii) Kutekeleza kikamilifu maazimio na maelekezo ya Mkutano Mkuu;

iii) Bodi itachagua kamati mbalimbali zitakazosimamia ufanisi wa kazi za maendeleo ya chama na kamati hizo zitakuwa

chini ya Bodi;

iv) Kuandaa na kutunza Hesabu za Chama kwa usahihi na kwa wakati;

v) Kutunza kwa usahihi daftari la wanachama na kumbukumbu za mihtasari ya Mikutano Mikuu na Vikao vya Bodi;

vi) Kuhakikisha kuwa lakiri ya chama inakuwepo na inatumika ipasavyo;

vii) Kufanya maamuzi kuhusu udahili wa wanachama wapya, kujiuzulu wanachama, kusimamishwa uanachama na kusimamishwa kwa wajumbe wa Bodi na kuwasilisha masuala hayo kwenye Mkutano Mkuu kwa ajili ya kujadiliwa na kutolewa maamuzi ya mwisho;

viii) Kubuni na kutayarisha Sera na kanuni mbalimbali zinazohusiana na shughuli za chama ili kufanikisha madhumuni ya chama.

ix) Kuandaa na kuwasilisha kwenye Mkutano Mkuu taarifa ya hali ya uchumi na maendeleo ya chama pamoja na hesabu ya mapato na matumizi, mizania iliyothibitishwa kwa mwaka uliopita na makisio ya mapato na matumizi kwa mwaka unaofuata;

x) Kupokea na kujadili taarifa za Kamati mbalimbali zinazosimamia kufanya kazi ili ushauri na kutoa mapendekezo kwa ajili ya kufanyiwa kazi kwa wakati;

xi) Kupitia, kujadili na kutolea maamuzi maombi ya vyama kwa ajili kujiunga na Chama Kikuu;

xii) Kuteua mwanachama atakayeshika nafasi iliyoachwa wazi katika Kamati mbalimbali zilizoundwa na mjumbe aliyeteuliwa atashika nafasi hiyo mpaka Mkutano Mkuu mwingine unaofuata ambapo nafasi iliyoachwa wazi itajazwa kwa kupigiwa kura au kwa uthibitisho;

xiii) kumwezesha mtu aliyeidhinishwa kukagua vitabu vya chama na kuhakikisha kuwa hatua zinachukuliwa kutokana na Taarifa ya ukaguzi;

xiv) kumwezesha MENEJA MKUU kutekeleza majumu yake ikiwa ni pamoja na kuweka taratibu za kuwakopesha watumishi, wajumbe wa Bodi na mwanachama wa UNION chini ya maelekezo ya Bodi kupitia sera ya utumishi;

xv) kuhakikisha kuwa wanachama wanafuata na kuzingatia Masharti haya, taratibu, mikataba na miongozo mbalimbali;

xvi) kufungua akaunti Benki na kuhakikisha kuwa fedha zote

za chama kikuu zinatunzwa katika benki;

xvii) kujadili na kuweka mipango ya namna ya kutekeleza Sera ya Maendeleo ya Ushirika;

xviii) kuandaa mpango mkakati, mpango wa biashara na programu ya utekelezaji wake;

xix) kuhakikisha kwamba chama kinawakilishwa katika mashitaka yoyote;

xx) kuhakikisha kuwa mali, bidhaa, vifaa na nyaraka/Hati za Chama zinahifadhiwa vizuri na kwa usalama;

xxi) kuteua watia saini kwenye hundi za chama;

xxii) kuajiri na kuteua watumishi wenye sifa za kutosha kutenda shughuli za Chama wakiwemo Meneja Mkuu, Meneja shughuli, Mhasibu, Mweka Hazina, au watumishi wengine miongoni mwa wanachama au nje ya wanachama ambao wataendesha shughuli za kila siku za chama;

xxiii) kuingia mikataba mbalimbali kwa niaba ya chama kwa kuzingatia Kanuni za Vyama vya Ushirika;

xxiv) kuhakikisha kuwa wakopaji wanalipa madeni yao kama walivyoahidi na kuwachukulia hatua za kisheria wakopaji

wasio waaminifu;

xxv) kupendekeza kwenye Mkutano Mkuu ufutaji wa mikopo mibaya ambayo haiwezi kulipwa kabisa kwa kuzingatia Kanuni za vyama vya ushirika;

xxvi) kupendekeza kwenye Mkutano Mkuu mabadiliko au viwango vya riba au masharti ya ulipaji mikopo ya vyama wanachama (amortization);

xxvii) kuandaa marekebisho ya masharti ya chama pale itakapobidi na kuwasilisha kwenye Mkutano Mkuu kwa ajili ya kujadiliwa na kutolewa maamuzi;

xxviii) Kuwasilisha kwa Mrajis mikataba yote ya kibiashara iliyoingiwa na chama kwa ajili ya kusajiliwa;

xxix) kusimamia utekelezwaji wa shughuli za chama kwa kumtaka Meneja Mkuu/Katibu kutoa taarifa ya matokeo ya uendeshaji wa shughuli za chama;

xxx) kuchapisha Hati za kumiliki hisa kwa ajili ya wanachama;

xxxi) kuandaa mipango ya uwekezaji na kuiwasilisha kwenye Mkutano Mkuu kwa ajili ya kujadiliwa na kutolewa maamuzi;

xxxii) Kufanya mambo mengine yote ambayo yataonekana ni lazima katika kutimiza madhumuni ya chama kwa

kuzingatia Sheria za nchi.

xxxiii) Kuwasilisha taarifa za shughuli za chama kama itakavyoelekezwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika.

Kazi za Mwenyekiti wa Bodi ya Uongozi

48 Mwenyekiti wa Bodi atapaswa kutekeleza kazi zifuatazo: -

a) Kuongoza vikao vyote vya Bodi ya Chama;

b) Kwa kushirikiana na Katibu kuitisha Mikutano Mikuu na vikao vya Bodi kwa kuzingatia Sheria ya Vyama vya Ushirika, 2013, Kanuni zake na Masharti haya;

c) Kutia saini kumbukumbu za vikao vya Bodi;

d) Kutia saini kwa niaba ya Chama, kumbukumbu zote ikiwa ni pamoja na zinazohitaji kuwekwa lakiri na/au muhuri wa Chama;

e) Kuwa msemaji mkuu wa Chama, kama haitaamriwa vinginevyo na Bodi au Mkutano Mkuu wa wanachama.

Kazi za Makamu Mwenyekiti

49 Makamu Mwenyekiti atapaswa kutekeleza kazi zote za Mwenyekiti endapo Mwenyekiti hatakuwepo.

Sifa za Mjumbe wa Bodi

50 Mjumbe wa Bodi ya Uongozi na wa Kamati ya Usimamizi lazima awe na sifa zifuatazo: -

a) Awe na elimu ya angalau kidato cha nne;

b) Awe mwadilifu na mwaminifu;

c) Awe ni mjumbe mwakilishi wa Chama cha Msingi wa Mkutano Mkuu wa Chama;

d) Awe na uwezo wa kuongoza;

e) Awe ametimiza matakwa ya sharti la 15 (1) (b) na 15 (2) la Masharti haya kuhusu ulipaji wa hisa;

f) Awe hajawahi kupoteza sifa za uongozi katika ngazi yoyote ya Chama kikuu na chama cha Ushirika;

g) Awe hajawahi kuwa mjumbe wa Bodi iliyoshindwa kusimamia vizuri shughuli za chama kikuu/msingi na kikapata hasara;

h) Awe anashiriki kikamilifu katika shughuli zote za chama kikuu.

i) Hajawahi kusababisha hasara katika chama chochote cha ushirika;

j) Asiwe na tabia ya kulaza madeni; na

k) Awe na sifa ya elimu kama zilivyoelekezwa na sheria ya Vyama vya Ushirika.

l) Awe ametoka kwenye chama cha msingi kilichokamilisha

hisa za msingi na kiwe na akiba isiyopungua 100,000/=

m) Asiwe na biashara inayofanana na shughuli za chama kikuu au chama cha msingi anachotoka.

Meneja Mkuu wa Chama

51 (1) Bodi ya chama kwa kushauriana na Mrajis, Mrajis Msaidizi au afisa ushirika wa wilaya itaajiri mtu mwenye sifa ya kuwa Meneja Mkuu wa Chama ambaye atawajibika kwa Bodi ya uongozi wa chama.

(2) Meneja/Katibu wa chama atakuwa ndiye msimamiaji wa shughuli zote za Chama za kila siku kulingana na miongozo itakayotolewa na Bodi na pia atakuwa katibu wa vikao vya Bodi.

(3) Majukumu ya Meneja Mkuu wa chama ni kama ifuatavyo: -

(a) kutekeleza na kuzingatia Sheria ya Vyama vya Ushirika na Kanuni zake, Sera ya Maendeleo ya Ushirika, Masharti haya, Kanuni na Sera mbalimbali zilizowekwa kwa ajili ya kuongoza utekelezaji wa shughuli za chama;

(b) kuhakikisha mifumo ya utendaji na utoaji taarifa ipo madhubuti na inawezesha mawasiliano;

(c) kwa kushauriana na Wajumbe wa Bodi, kuandaa mpango mkakati, mpango biashara, bajeti ya mwaka na program ya utekelezaji;

(d) atakuwa mtumishi na MTENDAJI MKUU wa chama;

(e) atafanya mawasiliano yote kwa niaba ya chama;

(f) kutayarisha/kuandaa mipango ya maendeleo ya muda mfupi na muda mrefu ya Chama;

(g) kutayarisha taarifa za Chama za mwezi, robo, nusu na mwaka mzima;

(h) kuhakikisha malengo na shabaha za Chama zinafikiwa;

(i) kushughulikia masuala yote yanayowahusu watumishi, hususan mafunzo na uendelezaji wa rasilimali watu;

(j) kwa kushirikiana na Wajumbe wa Bodi, kukiwakilisha Chama katika shughuli na uingiaji wa mikataba yote ya biashara;

(k) kuhakikisha vitabu vya hesabu vinaandikwa na hesabu zinaandaliwa na kuwasilishwa kwa Wakaguzi kwa wakati;

(l) kuhakikisha taarifa ya mapato na matumizi, mizania, na taarifa ya mikopo iliyochelewa zimeandaliwa kwa usahihi na wakati;

(m) kutoa taarifa za menejimenti kwenye vikao vya Bodi ambazo zinaeleza hali ya kifedha ya Chama ikianisha mizania, hesabu ya mapato na matumizi, taarifa ya mikopo

iliyochelewa, bajeti ya mwaka, mwenendo wa Chama na uwiano wake;

(n) kuidhinisha matumizi yaliyoko kwenye makisio kwa viwango vilivyowekwa na Bodi na kutia saini kwenye nyaraka zinaruhusu utoaji fedha za Chama kwa kuzingatia ukomo ulioainishwa kwenye sera za chama;

(o) kuisaidia Bodi kupanga viwango stahiki vya riba, ada na gharama nyingine kwa bidhaa na huduma zitakazotolewa;

(p) kuisaidia Bodi katika kubainisha dhamana zinazokubalika na zinazoweza kutumika kudhamini mikopo;

(q) kuhakikisha kuwa kuna ukwasi wa kutosha kukidhi mahitaji ya mikopo, uchukuaji wa akiba na gharama za uendeshaji;

(r) kusimamia ufunguwaji na uendeshwaji wa akaunti;

(s) kuajiri na kuwafukuza kazi watumishi walioko katika mamlaka yake, na baadae kuidhinishwa na bodi, kulipa stahili za watumishi kama zitakavyoidhinishwa na Mkutano Mkuu, kuwatuza na kuwapandisha vyeo watumishi au kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi wakosaji kwa kuzingatia sera ya utumishi;

(t) kutoa taarifa stahiki kwa mamlaka zinazohusika kwa muda

muafaka;

(u) kutekeleza mapendekezo yanayotolewa kwenye taarifa za Wakaguzi wa Ndani na wa Nje na taarifa za kiuchunguzi zinazotolewa na mamlaka husika; na

(v) kufanya kazi na majukumu mengine kadri ya maelekezo ya Bodi.

Kamati mbalimbali za Usimamizi

52 (1) Kutakuwa na Kamati ya mbalimbali za Usimamizi wa Chama ambazo zitakuwa na wajumbe wasiozidi watatu watakaochaguliwa na Mkutano Mkuu na hawapaswi kwa wakati mmoja kuwa Wajumbe wa Bodi. Kamati hizi zitawajibika kwa wanachama.

(2) Wajumbe wa Kamati za Usimamizi watahudumu katika nafasi hiyo kwa kipindi cha miaka mitatu na wanaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu.

(3) Wajumbe wa Kamati za Usimamizi watachagua Mwenyekiti na Katibu kutoka miongoni mwao. Katibu atatunza kumbukumbu zote za vikao vya Kamati ya Usimamizi.

Kazi za Kamati mbalimbali za Usimamizi

53 Kamati ya Usimamizi itapaswa kutekeleza kazi zifuatazo: -

(a) kufanya mapitio ya mara kwa mara kuhusu usahihi wa kumbukumbu za hesabu;

(b) kutoa taarifa kwenye kila kikao cha kawaida cha Bodi;

(c) kutoa mapendekezo ya kuboresha Sera, taratibu za uendeshaji na udhibiti wa ndani na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wake;

(d) kuandaa taarifa ya ukaguzi na usimamizi wa hesabu ya mwaka na kuiwasilisha kwenye Mkutano Mkuu wa mwaka kama Mkaguzi wa nje hataweza kufanya hivyo;

(e) kupendekeza kwa Bodi wakaguzi wa nje watakaofanya ukaguzi kwa mwaka wa fedha unaofuata endapo sio COASCO;

(f) Kusimamia fedha na mali zote za chama kwa niaba ya wanachama.

(g) Kufuatilia maendeleo ya miradi mikubwa ya Chama

(h) Kutafuta ufumbuzi wa masuala mbalimbali ya kiuongozi na kushauri Mkutano Mkuu ipasavyo; na

(i) kutekeleza majukumu mengine kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika na sheria nyingine pamoja na kanuni zake.

Ajira katika chama

54 (1) Chama kitaajiri au kuazima watumishi wenye ujuzi

unaotakiwa katika kutekeleza kazi za chama ambazo ni pamoja na: -

a) Menejimenti na utawala.
b) Uhasibu/uandishi wa vitabu vya hesabu.
c) Kazi za muda maalumu.
d) Kazi nyinginezo

(2) Watumishi wanaoweza kuajiriwa au kuazimwa ni pamoja na Meneja, Mhasibu, Mkaguzi wa Ndani, Wanasheria au watu wengine kadri itakavyohitajika.

Mkaguzi wa ndani

55 Chama kitaajiri mkaguzi wa ndani kwa ajili ya kuongeza udhibiti wa ndani na atawajibika kwa bodi.

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA

## UANDAAJI WA SERA NA MIONGOZO YA CHAMA

Chama kuandaa Sera na miongozo

56 Chama kitaandaa sera na miongozo mbalimbali kama ilivyoelekezwa kwenye Kanuni ya Vyama vya Ushirika. Miongozo hiyo ni pamoja na: -

i. Sera ya uhifadhi kumbukumbu
ii. Sera ya Ukwasi, Mali na Dhima
iii. Sera ya Uwekezaji
iv. Mwongozo wa usimamizi wa majanga
v. Sera ya udhibiti wa ndani

vi. Sera ya utumishi
vii. Kanuni za fedha na uhasibu
viii. Mpango mkakati na mpango kazi.
ix. Makisio ya mapato na matumizi (Bajeti) ya kila mwaka

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI

## KUFUTWA NA UFILISI WA CHAMA

Sababu za kufutwa

57 (1) Chama inaweza kufutwa: -

i. Kwa amri ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika

ii. Kwa maombi ya wanachama wasiopungua robo tatu (3/4) ya wanachama wote; na

iii. Iwapo tu wanachama wamepungua na kuwa pungufu ya idadi ya chini inayokubalika kisheria.

iv. Chama kushindwa kujiendesha miezi sita mfululizo.

Ufilisi

58 (1) Ufilisi wa Chama utafanywa kwa kufuata utaratibu kama ulivyoainishwa chini ya Sheria.

(2) Pale ambapo Mfilisi atakuwa amekamilisha ufilisi na kuwa amewalipa wadai wote wa chama, bakaa ya fedha za chama zitagawiwa kwa waliokuwa wanachama wa Chama wakati wa kufutwa kwake kwa uwiano ulio sawa.

## SEHEMU YA KUMI NA TATU
## MASHARTI MENGINEYO

Viongozi kutunza siri

59 Wajumbe wa Bodi, Watendaji Wakuu na watumishi wa Chama watapaswa kutunza **SIRI** kuhusu kumbukumbu zote za maisha ya mwanachama binafsi, isipokuwa masuala ya utoaji na ukusanyaji wa mazao ambayo Bodi inaweza kuchukua hatua zozote za lazima dhidi ya wanachama.

Msemaji wa Chama

60 Mwenyekiti ndie atakuwa msemaji wa chama

Mihuri ya Chama

61 Chama kitakuwa na mihuri ya mpira na ya lakiri ambayo itatunzwa na Meneja wa chama na itaifadhiwa kwenye kasiki la chama. Lakiri ya chama itatumika katika mikataba ya chama.

Chama kuungana na taasisi nyingine

62 (1) Chama kinaweza kuungana na chama kingine cha ushirika kuanzisha Mradi wa Pamoja wa ushirika au kuungana na kampuni au taasisi nyingine isiyo ya ushirika kuanzisha Ubia wa Pamoja.

(3) Chama kinaweza kuungana na Vyama vingine na kuunda Shirikisho la Vyama vya Ushirika.

Bima ya mali na fedha

63 Chama kitakuwa na wajibu kuhakikisha usalama wa

za chama — mali na fedha kwa kukata bima.

Mabadiliko ya Masharti — 64 Masharti haya yanaweza kubadilishwa kwa kufuata taratibu zilizowekwa na Sheria ya Vyama vya Ushirika, 2013 na Kanuni zake na hayatakuwa halali kutumika mpaka yatakapoidhinishwa na kusajiliwa na Mrajis.

Utatuzi wa migogoro — 65 (1) Mgogoro wowote unaohusu shughuli za Chama kati ya wanachama wake au watu wanaowalalamikia, au kati ya mwanachama au watu ambao wanadai na Bodi au Afisa yeyote, au kati ya Chama na chama cha ushirika kingine au Mtoa Huduma utasuluhishwa kwa njia ya amani kupitia majadiliano au maridhiano.

(2) Ikiwa mgogoro chini ya sharti dogo la (1) haujasuluhishwa kwa amani ndani ya siku 30, mgogoro huo utapelekwa kwa Mrajis kwa usuluhishi kupitia Fomu Na. 13 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2015.

(3) Kupelekwa kwa usuluhishi chini ya sharti dogo la (2) kunaweza kufanywa na Bodi au kwa azimio la Mkutano Mkuu au na mhusika yeyote katika mgogoro au na mwanachama yeyote wa Chama kama mgogoro unamhusu Mjumbe wa Bodi kudaiwa kiasi cha fedha na chama.

(4) Katika kupeleka mgogoro kwa Mrajis chini ya sharti dogo la (3), mlalamikaji atapaswa kupeleka nakala ya marejeo kwa ajili ya mlalamikiwa.

(5) Katika kupokea marejeo chini ya sharti dogo la (2),

Mrajis ataweka tarehe ya kupokea na kutuma nakala kwa mlalamikiwa na wahusika wote ambao kwa maoni yake mgogoro huo unawahusu.

(6) Baada ya kupokea marejeo ya mgogoro katika sharti dogo la (5), mlalamikiwa atapaswa ndani ya siku kumi na tano tokea tarehe ya kupokea, kuwasilisha maelezo ya kujibu kwa Mrajis.

(7) Taratibu nyingine za utatuzi wa migogoro baada ya hatua ya sharti dogo la (6) zitafanyika kwa kuzingatia Kanuni za WAMACU LTD

Mgongano wa tafsiri ya Masharti

**66** Endapo kutatokea mgongano kuhusu tafsiri ya Masharti haya, suala hili litapelekwa kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika kwa ajili ya maamuzi.

Utakatishaji fedha

**67** Chama kitaandaa miongozo na taratibu za ndani kwa ajili ya kubaini na kutoa taarifa dhidi ya vitendo vya utakatishaji wa fedha kama inavyoelekezwa kwenye Sheria ya kuzuia utakatishaji fedha.

Ulinzi wa mlaji

**68** Chama kitapaswa kuweka wazi upatikanaji wa huduma zitolewazo na chama na kuweka utaratibu wa kushughulikia malalamiko yatakayo jitokeza.

Uwasilishaji wa taarifa za wakopaji

**69** Chama kitawasilisha taarifa za wakopaji wazamani na wasasa kila mwezi kwa watoa huduma wa mfumo wa upashanaji wa taarifa za wakopaji (Credit Reference

Bureau).

Ulipaji wa riba na gawio

**70** Chama kitahakikisha kinalipa riba juu ya Akiba na Amana kwa wanachama pamoja na kutoa gawio kwa kuzingatia faida iliyopatikana kwa mwaka husika.

Masharti haya yamethibitishwa na wanachama wafuatao kwa niaba ya wanachama wote wa WAMACU LTD.

| Na. | Jina la Mwanachama | AMCOS | Na.ya SIMU | Saini | Tarehe |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | | |
| 2 | | | | | |
| 3 | | | | | |
| 4 | | | | | |
| 5 | | | | | |
| 6 | | | | | |
| 7 | | | | | |
| 8 | | | | | |
| 9 | | | | | |
| 10 | | | | | |
| 11 | | | | | |
| 12 | | | | | |
| 13 | | | | | |
| 14 | | | | | |
| 15 | | | | | |
| 16 | | | | | |
| 17 | | | | | |
| 18 | | | | | |
| 19 | | | | | |
| 20 | | | | | |

_________________________________

*Mrajisi wa Vyama vya Ushirika*

Tarehe_________________

| Na. | Jina la Mwanachama | AMCOS | Na.ya SIMU | Saini | Tarehe |
|---|---|---|---|---|---|
| 21 | | | | | |
| 22 | | | | | |
| 23 | | | | | |
| 24 | | | | | |
| 25 | | | | | |
| 26 | | | | | |
| 27 | | | | | |
| 28 | | | | | |
| 29 | | | | | |
| 30 | | | | | |
| 31 | | | | | |
| 32 | | | | | |
| 33 | | | | | |
| 34 | | | | | |
| 35 | | | | | |
| 36 | | | | | |
| 37 | | | | | |
| 38 | | | | | |
| 39 | | | | | |
| 40 | | | | | |

_________________________________

*Mrajisi wa Vyama vya Ushirika*

Tarehe________________

| Na. | Jina la Mwanachama | AMCOS | Na.ya SIMU | Saini | Tarehe |
|---|---|---|---|---|---|
| 41 | | | | | |
| 42 | | | | | |
| 43 | | | | | |
| 44 | | | | | |
| 45 | | | | | |
| 46 | | | | | |
| 47 | | | | | |
| 48 | | | | | |
| 49 | | | | | |
| 50 | | | | | |
| 51 | | | | | |
| 52 | | | | | |
| 53 | | | | | |
| 54 | | | | | |
| 55 | | | | | |
| 56 | | | | | |
| 57 | | | | | |
| 58 | | | | | |
| 59 | | | | | |
| 60 | | | | | |

____________________________

*Mrajisi wa Vyama vya Ushirika*

Tarehe________________

________________________